**JAMHURI YA KENYA** **SERIKALI YA KAUNTI YA MAKUENI**

## IDARA YA AFYA

## MKATABA WA HUDUMA KWA RAIA

### 1.0. MAONO
Mfumo wa afya wa hali ya juu na wenye ufanisi unaofikika, wenye usawa na wa nafuu kwa Wakenya wote.

### 2.0. ELEKEZO
Kukuza na kushiriki katika kutoa huduma za afya jumuishi na zenye kuendeleza ufanisi, kinga, tiba na kurekebisha tabia kwa Wakenya wote.

### 3.0. MAADILI YA MSINGI
- Kuzingatia mgonjwa/kuangazia mteja.
- Ushirikiano
- Utaalamu
- Uadilifu na uwazi
- Uvumbuzi/ubunifu na ubora
- Kutopendelea

### 4.0. KAZI/MAJUKUMU
Huduma za afya za kaunty zikiwa ni pamoja na, hasa:

1. Vituo vya afya na madawa ya Kaunti.
2. Huduma za ambulansi.
3. Kukuza matibabu ya msingi.
4. Kutoa leseni na kudhibiti shughuli za uuzaji wa chakula kwa umma;
5. Makaburi/mava, vyumba vya mazishi na kuchomea maiti; na
6. Refuse removal, refuse dumps and solid waste disposal.

## 5.0. HAKI ZA MTEJA

1. Haki ya kupata huduma zote zitolewazo katika idara.
2. Haki ya kupata taarifa na habari za matibabu kwa wakati ufaao.
3. Haki ya mawasiliano bora.
4. Haki ya maeneo bora.
5. Haki ya kufanya uamuzi kuhusu matibabu.
6. Haki ya usiri.
7. Haki ya matibabu bora.
8. Haki ya kufidiwa malalamiko
9. Haki ya huduma za dharura

## 6.0. WAJIBU WA MTEJA

1. Kuheshimu haki za wateja wengine/wagonjwa na wahudumu wa afya.
2. Kutoa habari za kweli ili kusaidia katika kuchunguza na kutambuliwa kwa matibabu.
3. Kufuata matibabu yaliyopendwa na kuripoti madhara yake.
4. Kujulisha wahudumu wa afya kuhusu matatizo yanayotarajiwa baada ya kupata matibabu.
5. Kutimiza wajibu wote wa kifedha.
6. Kuhakikisha mazingira safi na salama ili kukuza afya.
7. Kufuata kanuni na mkataba wa huduma zetu katika vituo vyetu vyote vya afya.

8. Kutoa ripoti/makataa ya huduma zetu.

## 7.0. HUDUMA ZINAZOTOLEWA

| HUDUMA | MAHITAJI (WAJIBU WA MTEJA) | ADA/MALIPO (Ksh) | MUDA WA HUDUMA |
|---|---|---|---|
| Meza/deski ya maelekezo | Ushirikiano | bure | Dakika 5 |
| Usajili wa huduma za wateja wasio wa kulazwa. | Kadi ya usajili- ujio wa kwanza<br>Stakabadhi za kujitambulisha (Kitambulisho/pasipoti) | Shilingi 20 | Penye dharura: papo hapo<br>Pasipo dharura: Lisaa limoja |
| Usajili wa huduma za afya kwa wote | Stakabadhi za kujitambulisha (Kitambulisho, Cheti cha kuzaliwa) | Shilingi 500 kwa kila boma | Dakika 15 |
| Mashauriano:<br>Mtu mzima / Watoto wa miaka 5 na zaidi<br>Watoto wa miaka chini ya 5 | Kadi ya mgonjwa | Bure | Dakika 20 |
| Huduma za maabara | Fomu ya kuomba uchunguzi<br>Kulipia vipimo | Shilingi 50-1,500 kwa kila kipimo | Dakika 15 - hadi masaa 72 |
| Huduma za rediolojia | Fomu ya kuomba uchunguzi<br>Kulipia vipimo | Shilingi 200-2,000 | Dakika 15 - hadi lisaa limoja |
| Kulazwa kwa Wagonjwa (Baada ya dakitari kutoa uamuzi wa kumlaza mgonjwa hadi kwa wadi) | Mapendekezo ya daktari ya kulazwa<br>Stakabadhi za kujitambulisha (Kitambulisho/ pasipoti) Malipo ya faili | Shilingi 50-40,000 | Penye dharura: papo hapo<br>Pasipo dharura: Dakika 30- hadi masaa 3 |
| Huduma za figo | Kadi ya matibabu yenye tarehe iliyopangwa<br>Malipo ya amana | Kutegemea na utaratibu uliopo (7,500-15,000) | Penye dharura- dakika30<br>Kwa hiari kama ilivyohifadhiwa |
| Huduma za Kitengo cha Wagonjwa Mahututi | Kadi ya mgonjwa | Shilingi 500-40,000 | Penye dharura – dakika 30<br>Kwa hiari kama ilivyohifadhiwa |
| Viliniki Spesheli (ENT, Lishe, Matibabu ya macho, matibabu ya akili, GOPC, MOPC, SOPC,) | Mapendekezo ya Matabibu<br>Kadi ya matibabu<br>Risiti ya malipo | Shilingi 50-100 | Lisaa limoja |
| Madawa | Maelezo | Shilingi 20-2,500 | Dakika 30 |
| MCH/Kupanga uzazi | Kitabu au kadi ya Mama na mtoto | Shilingi 20-500 | Dakika 5-30 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Huduma zote kwa watoto chini ya miaka 5 ni bure | |
| Kliniki cha wajawazito | Kijitabu cha mama na mtoto | Bure | Dakika 30 |
| Huduma za uzazi | Kadi ya mteja | Bure | Inategemea na uchungu wa leba unavyokuwa<br>-6 Hours |
| Upasuaji | Kadi ya matibabu yenye tarehe iliyopangwa<br>Malipo ya amana | Kutegemea na utaratibu wa upasuaji (750-6000) | Penye dharura- dakika 30<br>Kwa hiari kama ilivyohifadhiwa |
| Upasuaji mdogo | Kadi ya mgonjwa | Shilingi 500 | Lisaa limoja |
| Huduma za meno | Kadi ya mgonjwa | 50-6,000 | Dakika 45 |
| chanjo (Mara kwa mara) | Mgonjwa mgeni – Hakuna<br>Kuzuru tena – Kijitabu cha chanjo | Bure | Dakika 15 |
| Chanjo (wanaoshughulika na vilaji) | Ripoti ya uchunguzi wa daktari | 200-600 | Dakika 15 |
| Huduma za urekebishaji | Kadi ya mgonjwa | 40-2,000 | Lisaa limoja |
| Kupunguza maumivu | Kadi ya mgonjwa | 50-100 | Lisaa limoja |
| Utibabu wa kisheria | Kadi ya mgonjwa<br>Fomu ya P3 | 500-1000 | Lisaa limoja |
| Huduma za chumba cha kuhifadhia maiti (mochari<br>kuimarisha mwili baada ya kufa/ Kibali cha kuhifadhi mwili) | Kulipa malipo | Shilingi 50 - 2,500 kwa kila huduma | Lisaa limoja |
| Ukaguzi wa vyumba vya biashara (kila mwaka) | Bila hitaji | 1,000 | Dakika 30 |
| Cheti cha wauzaji wa vilaji (kila mwaka) | Bila hitaji | 200 | Dakika 30 |
| Ukaguzi shuleni (kila mwaka) | Bila hitaji | 3,000 | Dakika 30 |
| Kliniki ya kipekee (kila mwaka) | Wageni – Bila hitaji<br>Waliopo – Leseni ya hapo awali<br>Fomu ya kuomba leseni | 3,000 | Lisaa limoja |
| Kutoa leseni za vinywaji vya pombe | Kibali cha afya ya umma | 1,000 | Dakika 20 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Kibali cha KRA | | |
| Rufaa za jamii | Fomu ya rufaa | Bila malipo | Lisaa limoja |
| Rufaa kati ya vituo vya afya | Fomu ya rufaa | 4,000-9,000 | Lisaa limoja |
| Ufuatiliaji na usimamizi wa kuzuka kwa magonjwa | Viwango vya vipimo | Bila malipo | Wiki moja |
| Malipo kwa wauzaji | Nakala ya ombi ya ununuzi/utaratibu wa huduma, Nambari ya utoaji na maelezo ya ripoti ya kupokea bidhaa, Maelezo ya ankara na benki | Bila malipo | Lisaa limoja |
| Maoni ya wateja | Mapendekezo / malalamiko | Bila malipo | Shukrani: siku 3 za kazi<br>Azimio: Siku 21 za kazi |

**Mbinu za kutoa maoni**

Tuma malalamiko na maoni yako kupitia kwa:

Eneo la mapokezi katika afisi za idara ya afya

Vijisanduku vya maoni vilivyoko ofisini mwetu kote.

tovuti: county.health@makueni.go.ke/co.health@makueni.go.ke

Afisa Mkuu – Huduma za Afya

S.L.P. 89-90300, Makueni